



Alikuwa kituamrisha tunapokuwa safarini tusivue khofu zetu kwa siku tatu (mchana na usiku) isipokuwa kwa ajili ya janaba, lakini ni kwa haja kubwa na ndogo na usingizi

Kutoka kwa Zirri bin Hubaishi amesema: Nilikwenda kwa Swafwan bin Assali Al-Muraadi, ili nimuulize kuhusu kufuta juu ya khofu mbili, akasema: Ni nini kimekuleta ewe Zirri? Nikasema: Kutafuta elimu, akasema: Hakika Malaika huweka mbawa zao kwa mwenye kutafuta elimu; kwa kuridhishwa na kile anachokitafuta, basi nikasema: Hakika mimi nimepata uzito ndani ya kifua changu kuhusu kufuta juu ya khofu mbili baada ya kukidhi haja ndogo na kubwa, na wewe ulikuwa miongoni mwa wanafunzi wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake, hivyo nimekuja kukuuliza: Je, uliwahi kumsikia akizungumza chochote kuhusu hilo? Akasema: Ndiyo, Alikuwa kituamrisha tunapokuwa safarini tusivue khofu zetu kwa siku tatu (mchana na usiku) isipokuwa kwa ajili ya janaba, lakini ni kwa haja kubwa na ndogo na usingizi, nikasema: Je, uliwahi kumsikia akizungumza chochote kuhusu matamano? Akasema: Ndiyo, tulikuwa pamoja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika safari, wakati tukiendelea kuwa naye ghafla, Bedui mmoja alimuita kwa sauti kubwa na ya juu. Ewe Muhammadi!!!, Mtume rehema na amani ziwe juu yake akamjibu kwa mfano wa sauti yake: "Ehee, niambie!" Tukasema kumwambia koma!, punguza sauti yako, kwani hapa uko mbele ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na umekatazwa kufanya hivi, akasema: Wallahi siwezi kupunguza, kisha Bedui akasema: Utakuta mtu anawapenda watu fulani lakini hajawahi kukutana nao, akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Mtu atakuwa pamoja na yule anayempenda siku ya Kiyama" Basi akaendelea kutusimulia mpaka akautaja mlango ulioko Magharibi mwendo wa upana wake, au anaweza kutembea aliyepanda kwenye upana wake kwa miaka arobaini au sabini.

[Sahihi] [Imepokelewa na Tirmidhiy, Ibn Majah na Ahmad]

Alikuwa Zirri bin Hubaishi kwa Swafwan bin Assali radhi za Allah ziwe juu yake, ili amuulize kuhusu khofu mbili, Swafwan akasema: Ni nini kimekuleta ewe Zirri? Akasema: Kutafuta elimu, akasema: Hakika Malaika huweka mbawa zao kwa mwenye kutafuta elimu; kwa kuridhishwa na kutukuza kile anachokifanya mwenye kutafuta elimu, Zirri akasema: Hakika nimepata shaka ndani ya nafsi yangu kuhusu kufuta juu ya khofu mbili baada ya haja kubwa na ndogo, na wewe ni katika Maswahaba wa Mtume rehema na amani ziwe juu yake na nimekuja hapa kukuuliza, je, uliwahi kumsikia Mtume rehema na amani ziwe juu yake akitaja chochote kuhusu hili?. Akasema Swafwan: Ndiyo, alikuwa akituamrisha tunapokuwa wasafiri tusivue khofu zetu kwa siku tatu (mchana na usiku) kwa sababu ya hadathi (uchafu) mdogo,

kama haja kubwa nandogo na usingizi, isipokuwa janaba hapo basi ni wajibu kuvua, nikasema: Je, uliwahi kumsikia akizungumza chochote kuhusu mapenzi? Akasema: Ndiyo: Tulikuwa pamoja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake katika safari, wakati tukiwa bado tuko pamoja naye mara ghafla Bedui mmoja aliita kwa sauti ya juu sana: Ewe Muhammadi!, Mtume rehema na amani ziwe juu yake akamjibu kwa sauti ya juu karibu na sauti yake: Njoo, nasi tukasema kumwambia: Koma! Shusha sauti yako, kwani hapa uko mbele ya Mtume rehema na amani ziwe juu yake, na umekatazwa kunyanyua sauti mbele yake. Akasema kwa sababu ya ukaidi wake: Wallahi siwezi kuishusha, Bedui akasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, utakuta mtu anawapenda watu wema na hajafanya matendo mfano wa matendo yao? Akasema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Mtu atakuwa pamoja na anayempenda siku ya Kiyama, Anasema Zirri: Swafwan akaendelea kutuhadithia mpaka akataja mlango wa toba ulioko upande wa Sham aliuumba Mwenyezi Mungu siku aliyoumba Mbingu na Ardhi, anaweza kutembea aliyepanda juu ya kipando kwenye upana wake miaka arobaini au sabini, na wala haufungwi mpaka Jua lichomoze kutokea Magharibi yake.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/4565>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

